
Jarida la Kiswahili Sanifu




# Uchanganuzi Kisemiotiki wa Matini za Kombe la Dunia 2022 katika Gazeti la Taifa Leo

Videlis Lusweti[a*], Frida Miruka[a], Benard Okal[b]

*Elimu ya Lugha na Fasihi, Shule ya Sanaa na Sayansi ya Jamii, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kakamega, Kenya.*

*Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Maseno, Maseno, Kenya.*

**IKISIRI**

Matini za kombe la dunia 2022 zilishuhudia matumizi ya ishara mbalimbali zilizobeba ujumbe muhimu kwa hadhira. Ingawa zingine zilikuwa za moja kwa moja, nyingi zilisetiri ujumbe ambao haungeweza kufasiriwa moja kwa moja na wasomaji. Lengo la makala haya ni kuchanganua matini za Kombe la dunia 2022 katika gazeti la Taifa Leo kisemiotiki ili kuweka wazi ujumbe uliolengwa. Makala imejikita katika nadharia ya semiotiki iliyoasisiwa na Saussure (1946) inayoshughulikia ishara na uashiriaji na maana zao katika matini za kifasihi na isimu. Utafiti uliofanyika ulilenga matini kuhusu kombe la dunia katika Gazeti la Taifa Leo. Sampuli ya kimaksudi ilitumika kuteua matini za kisemiotiki kwa mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo.Dta ilikusanywa kwa udurusu wa magazeti ya Taifa leo, kuchanganuliwa na kuwasilishwa kwa maelezo na madondoo ya matini za kisemiotiki. Makala inaonyesha kuwa kategoria tatu za matini za kisemiotiki za picha, maelezo na matini za kitamathali zilitumika. Ujumbe katika matini hizi ulijitokeza katika uashiriaji kisemiotiki na ulihusu uovu wa jamii (rangi nyeusi); hatari (wekundu); amani (weupe); utamu (asali), utamaduni, dini pamoja na masuala ya uchumi na biashara. Utafiti unapendekeza kuwa waandishi waimarishe sanaa na uandishi kwa kutumia mbinu na mitindo zaidi ya kisemiotiki ili kuweka wazi ujumbe wa matini za kitaaluma.

**KUHUSU MAKALA**

*Maneno Muhimu:*
Gazeti la Taifa Leo,
Kombe la Dunia,
Semiotiki.

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 24 Februari 2026
Tarehe ya Kurekebishwa: 7 Mai 2026
Tarehe ya Kukubalika: 7 Mai 2026
Mtandaoni: 31 Julai 2026

## 1. Utangulizi

Vyombo vya habari vikiwemo magazeti hutelekeza wajibu muhimu kupasha ujumbe kwa umma kuhusu matukio makuu ulimwenguni. Vile vile huelimisha, hutaarifu na kutumbuiza hadhira kubwa (Singh & Nity 2017). Vyombo vya habari vikiwemo magazeti vina wajibu muhimu wa kujenga mitazamo, tabia na mielekeo ya wanajamii. Ili kutekeleza wajibu huu ipasavyo, ujumbe unaowasilishwa kupitia vyombo mbalimbali sharti uwe wazi kwa hadhira. Maana na ujumbe wa matini za kisemiotiki huchambuliwa kutumia nadharia ya semiotiki ambayo hushughulikia ishara, alama na maana katika muktadha wa kijamii au kiutamaduni. Matini inaweza kuwa maandishi, picha, au aina yoyote ya mawasiliano inayotumia alama.

Kwa mujibu wa Kress na Leeuwen (2010) katika nadharia yao ya Muundo wa ishara wanasema kuwa ishara hujengana katika kutoa maana inayokusudiwa na muundaji wa picha hiyo. Lugha hueleza ujumbe kwa ufupi huku picha zikitoa ufafanuzi kwa njia isiyo wazi na inayowapendeza watazamaji. Miongoni mwa vipengele muhimu ambavyo vilishughulikiwa kufasiri ujumbe ni maana ya maneno, ishara mbalimbali, hadhira lengwa, uhusiano wa wahusika, mahali, elementi mbalimbali zimewekwa kwenye picha pamoja na vitendo. Kutokana na maelezo haya utafiti huu ulilenga vipengele hivi ili kutoa maana na ujumbe ambao ulijitokeza kwenye matini mbalimbali za kisemiotiki katika gazeti la Taifa Leo. Vipengele hivi vyote vinatumiwa kutoa maana na ujumbe kisemiotiki jinsi ambavyo Heather na Noxol (2014) wanaeleza kuwa maana hujitokeza kwa kuzingatia hisia za mtu, imani au mawazo ambayo yameambatanishwa na kiashiria. Vitu kama rangi, nguo, maneno au ishara za kimwili huchangia pakubwa wakati hadhira inatfsiri maana katika picha. Pia, taswira huchanganuliwa kwa kiwango cha maelezo bila kuchunguza kwa kina maana inayokusudiwa.

Picha huweza kuelezwa bila kuitathmini au kutoa maelezo ya ndani. Hivyo basi, kombe la dunia 2022 ni miongoni mwa matukio makuu yaliyozingatiwa na umma katika uwanja wa michezo hata hivyo ujumbe wake uliwasilishwa kwa njia nyingi ikiwemo matumizi mengi ya ishara baadhi yazo zikibeba mzigo mzito wa

*Mwandishi Mkuu. Barua Pepe: vlshadrack@gmail.com

Mhariri: Leonard Mwita, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
Nukuu: Lusweti V., Miruka F., & Okal B. (2026). Uchanganuzi Kisemiotiki wa Matini za Kombe la Dunia 2022 katika Gazeti la Taifa Leo. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(2), 10 – 17. https://doi.org/10.61889/rm8b6w06.

© 2026 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

kisemantiki uliohitaji kufasiriwa ili kuwasilisha ujumbe kwa umma kwa ukamilifu.

### 1.1. Misingi ya nadharia

Makala hii inaongozwa na nadharia ya semiotiki iliyoasisiswa na Ferdinand Saussure (1946) na mwanafalsafa wa Kimarekani Charles Sanders Pierce (1996) mwanzoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 na baadaye Charles William Morris (1901-1979). Semiotiki ni taaluma ambayo huchunguza alama, ishara na mifumo ya maana inayotumika katika mawasiliano. Ferdinand de Saussure (1986) alieleza kuwa nadharia hii hutumika kuelewa jinsi ishara zinavyotengeneza maana katika muktadha wa kijamii, kitamaduni na kisanaa. Katika matini za kisemiotiki maana na ujumbe huzingatiwa kwa kuzingatia vipengele vya ala na ishara kama kitajwa na kitajika. Kitajwa ni wazo linalowakilishwa na kitajika ni umbo la ishara, kama neno, picha au sauti.

Saussure (1986) kwa upande wake alifafanua semiotiki kama taaluma ya uchunguzi wa ishara na dhima yake katika jamii. Kazi za Pierce kwa upande mwingine zilijikita katika pragmatiki na kimantiki ili zieze kuleta maana maalum. Kulingana na mawazo yake, ishara hutumiwa kufafanulia vitendo maalum na maana ya ishara hiyo inatokana na sheria fulani za utamaduni wa tanzu lugha. Unakidi wa ishara hufanyika katika utamaduni mahsusi ambapo mifumo ya ishara inajulikana, inatumiwa na kufahamika na wanajamii waliolelewa katika utamaduni huo maalum. Kazi za Pierce (2002) kwa upande mwingine zilijikita katika pragmatiki na kimantiki ili zieze kuleta maana maalum. Kulingana na mawazo yake, ishara hutumiwa kufafanulia vitendo maalum na maana ya ishara hiyo inatokana na sheria fulani za utamaduni wa tanzu lugha. Pierce alifafanua ishara kama 'kitu kinachosimama mahali pa kingine' Mchango wa Pierce mkuu ulikuwa kuainisha ishara katika makundi matatu; picha inayofanana na kiashiria, ishara ya maana fulani na ishara zinazoonekana zenye maana nyingine.

Makala haya yalitumia mihimili minne mikuu kuelezea nadharia hii, kwa mujibu wa Saussure (1986) alitazama ishara kama muunganiko wa vipengele viwili vikuu; kitambulisho inayoangazia sauti au umbo la neno na kitambulishi ambayo ni wazo linalowakilisha maana fulani. Naye Pierce (2002) alijikita kwa vipengele vitatu vikuu; taswira ambayo ni ishara inayofanana moja kwa moja na kitu; kisha kiashiria ambayo ni uhusiano wa karibu nayo alama huashiria maana inayotokana na makubaliano ya jamii. Barthes (1967) na Eco (1976) waliangazia maana kulingana na muktadha. Eco alieleza kuwa maana haipo ndani ya ishara yenyewe bali huzalishwa kutokana na muktadha. Mihimili hii ilikuwa muhimu kwa makala haya kwani matini zilizoangaziwa wakati wa kombe la dunia 2022 zilieza kufasiriwa ipasavyo na kupata maana iliyokusudiwa na hadhira. Pia, maana ilifafanuliwa kulingana na muktadha wa michezo ambao ulikuwa mhimili mkuu zaidi kwenye tafsiri ili wasomaji waeze kuelewa ishara hizo za picha na maelezo.

## 2. Uhakiki wa Maandishi

Sanja & Mbuthia (2025), katika uchunguzi kisemiotiki wa athari za kihistoria na mazingira kwa uchumi na maisha ya kijamii katika jamii za pwani wanafafanua ishara na tamathali za lugha kuhusu mazingira kwa kujikita katika misimbo ya Barthes (1957). Wanashadidia kuwa ufafanuzi wa ishara katika matini ni njia bora ya kuangazia ujumbe wa matini. Wataalum wengine wanaoangazia maana na ujumbe wa matini kisemiotiki ni Alvarez (2013), Heather na Nixol (2014), Jinshun (2019) na Arackal (2015).

Alvarez (2013) anasema kuwa usomaji wa semiotiki na mchakato wa mawasiliano huwa na hatua tatu zinazofuatana. Kwanza msomaji husoma tu ili kuelewa kile kinachowasilishwa kifasihi. Usomaji wa aina hii unahitaji mpangilio wa mchakato wa kuashiria, au kuiga, kama ishara za maneno humaanisha kile wanachosema. Msomaji anapaswa kuzingatia vipengele vyote vya muktadha, maandishi au yasiyo ya maandishi, anapojaribu kuunda upya maandishi yanayozunguka maadili yake mwenyewe kwa kuunda mfumo wake wa ishara (Derrida, 1997).

Heather & Noxol (2014) wanaeleza kuwa maana hujitokeza kwa kuzingatia hisia za mtu, imani au mawazo ambayo yameambatanishwa na kiashiria. Vitu kama rangi, nguo, maneno au ishara za kimwili huchangia pakubwa wakati hadhira inafasiri maana katika taswira. Pia, taswira huchanganuliwa kwa kiwango cha maelezo bila kuchunguza kwa kina maana inayokusudiwa. Picha huweza kuelezwa bila kuitathmini au kutoa maelezo ya ndani. Hivyo, tunaweza kupata maana kwa kurejelea matini. Matini katika muktadha huu huweza kuwa filamu, grafiti, mavazi, magazeti, mapambo au matangazo. Utafiti huu ulijikita katika matini za kisemiotiki katika gazeti la Taifa Leo (T.L) wakati wa kombe la dunia 2022.

Jinshun (2019) anahusisha Semiotiki kama mkabala wa uchanganuzi wa matini. Matini ni mkusanyo wa ishara (kama vile maneno, taswira, sauti na/au ishara) zilizoundwa (na kufasiriwa) kwa kurejelea kanuni zinazohusiana na aina na katika njia fulani ya mawasiliano. Tafiti za semiotiki huzingatia mfumo wa kanuni zinazotawala matini, zikisisitiza dhima ya muktadha wa semi katika kuunda maana. Semiotiki huzingatia muundo wa matukio ya kuleta maana, kwa ishara (ya maneno au isiyo ya maneno) kitengo cha msingi. Ishara (k.m. maneno, mavazi) huchanganyika na kuunda ujumbe na matini (k.m. maneno na sentensi).

Arackal (2015) anasema kuwa ni mwanasemiotiki wa Kifaransa Barthes (1980) aliyeonyesha kwanza umuhimu wa kusoma vyombo vya habari kulingana na jinsi vinaleta maana. Mbinu ya semiotiki ni ya msingi kwa sababu inalenga kwa karibu maana zilizofichika. Kama vile Mc Quail pia anavyosema, "Matumizi ya uchanganuzi wa semiolojia hufungua uwezekano wa kufichua zaidi maana ya msingi ya matini (yaliyomo)." Semiotiki inaweza kutumika kwa 'maandiko' ambayo yanahusisha zaidi ya mfumo mmoja wa ishara na ishara (kama vile taswira na sauti zinazoonekana).

## 3. Njia na Mbinu za Utafiti

Utafiti ulitumia muundo wa kifani ambao ulimwezesha mtafiti kushughulikia matini katika gazeti la Taifa Leo. Kwa mujibu wa Robert (2007), muundo huu humsaidia mtafiti kushughulikia jambo ambalo tayari analifahamu. Sampuli ya kimaksudi ilitumika kuteua magazeti ya Taifa Leo na matini ya kisemiotiki katika magazeti hayo wakati wa kombe la dunia 2022 kulingana na madhumuni ya utafiti (Palikan 2015). Hivyo basi,utafiti huu uliteua magazeti ya Taifa Leo kimaksudi. Vile vile taarifa kuhusu kombe la dunia ulilengwa ili kuteua matini ya kisemiotiki. Kwa mujibu wa Ennon (1998) anasema kuwa sampuli ya kimaksudi ni mwafaka kwa kuwa itarahisisha upatikanaji wa data za uhakika kwa muda mfupi kwani mtafiti hatatumia muda mwingi kufanya utafiti kwa kundi ambalo halihusiani na mada yake.

Utafiti ulikuwa wa maktabani na hivyo ulihusika na eneo la kitaaluma la uchanganuzi wa matini kisemiotiki kwa kuangazia vyombo vya habari. Hivyo basi, utafiti huu ulijikita katika uchanganuzi kisemiotiki wa matini za kombe la dunia katika gazeti la Taifa Leo wakati wa kombe la dunia 2022. Utafiti ulilenga magazeti ya Taifa Leo ya mwaka 2022. Data za sekondari zilikusanywa kutoka kwenye magazeti ya Taifa Leo yaliyokuwa na matini za kisemiotiki wakati wa K.L.D 2022. Mbinu na vifaa vilivyotumika katika ukusanyaji data ni udurusu wa matini, orodha ya ukaguzi pamoja na gazeti la Taifa Leo. Matini za kisemiotiki zilichanganuliwa na kufasiriwa ili kutoa maana kamili iliyokusudiwa. Orodha ya ukaguzi ilisaidia kuorodhesha magazeti ya T.L yaliyokuwa na matini za kisemiotiki za K.L.D 2022 tangu mchuano huo ulipoanza hadi kukamilika.Uchanganuzi wa data ulihusisha hatua sita ambazo ni: Upangaji, urekebishaji, uhariri, usimbaji, maelezo, pamoja na kuipa maana.

## 4. Matini za kisemiotiki za kombe la dunia 2022 katika magazeti ya Taifa Leo

Aina tatu za matini za kisemiotiki za kombe la dunia 2022 zilibainika katika Gazeti la Taifa Leo

### 4.1. Matini za picha

Matini za picha huhusisha taarifa au maandishi ambayo yameandikwa, kuchapishwa au kufinyangwa kwa njia inayojumuisha taswira au picha kwa lengo la kufikisha ujumbe fulani. Matini hizi zilihusisha picha ili kuongeza maana ya maandishi au kubeba ujumbe bila maneno mengi. Barthes (1980) alieleza matini za picha kupitia nadharia ya semiotiki kuwa picha hujumuisha viwango viwili vya maana: kwanza ni maana ya kimsingi ambayo ni ya moja kwa moja na ya pili ni maana ya kiashiria ambayo hutoa ujumbe wa ndani au tafsiri ambayo inaweza kuathiriwa na muktadha wa kijamii au kitamaduni. Kress na Leeuwen (1996) walionyesha kuwa picha zinasawiri mambo kama vile uhusiano, muundo, rangi pamoja na mitazamo. Manovich (2001) naye anasisitiza kuwa picha hasa za kidijitali zinaweza kuchukuliwa kama matini kwa maana zinatengenezwa na lugha fulani ambayo husaidia wasomaji kuzielewa na kuzitafsiri.




Tak. 1: *Novemba 19, 2022. Uk .13*

Katika Tak. 1 Makala inarejelea mwanamitindo Miss BumBum akiwa amevalia sare ya Barcelona huku mgongoni ikiwa imeandikwa nambari 10. Chini ya hii picha kuna kichwa cha nahodha wa kikosi cha Argentina Lionel Messi akiwa anatabasamu. Kando ya hizi picha kuna maelezo mafupi 'Miss BumBum aahidi Messi asali Argentina ikifana Qatar'. Licha ya huyu Miss BumBum kutoka nchi ya Brazil, amevalia vazi la Barcelona lenye nambari 10 mgongoni kuonyesha kuwa yeye ni shabiki sugu wa huyu mchezaji Messi ambaye alikuwa anachezea timu ya Barcelona kule Uhispania. Hivyo, aliamua kuendeleza ushabiki wake wakati wa michuano hii ya kombe la dunia kwa kuamua kuunga mkono nchi ya Argentina ili waweze kunyakua hilo taji licha ya nchi yake ya Brazil kuwa miongoni mwa mataifa ambayo yalikuwa yanapigiwa upato mkubwa wa kushinda. Picha hii ina ishara mbalimbali za kisemiotiki zenye ujumbe tofauti:

Maelezo *Miss BumBum aahidi Messi asali Argentina ikifana Qatar* yanaashiria usaliti wa nchi: kwanza inaonyesha kuwa Miss BumBum aliamua kumchagua Messi na kusaliti nchi yake ya Brazil. Maelezo haya yanaonyesha kwa kiwango gani huyu mwanamitindo yuko tayari kuenda na chenye atamfanyia huyu mchezaji iwapo wataweza kushinda hili kombe la dunia.

*Kuchanga njale za uso wake:* Ili kutimiza ahadi aliyokuwa amempa Lionel Messi, baada ya timu ya Argentina kushinda kombe la dunia 2022 nchini Qatar, Miss BumBum aliamua kuchanja njale za uso wa Messi kwenye makalio yake kama ishara ya kusherehekea ufanisi huo mkubwa.

*Kushabikia mchezaji Lionel Messi*: Pia, mwanamitindo huyu yuko na tattoo 3 kwenye mgongo wake za kuonyesha kuwa yeye ni shabiki sugu wa huyu mchezaji Lionel Messi. Moja inaeleza tawasifu yake, nyingine ina alama za dukuduku tatu kuashiria idadi ya vikombe za dunia ambazo nchi ya Argentina iliweza kunyakua na ya mwisho ni nambari 10 ambayo pia inaashiria nambari ya jezi ambalo mchezaji huyu huvalia akiwa uwanjani. Mwanamitindo huyu alifanya haya yote

ili kutimiza ahadi ambazo alikuwa amewapa mashabiki wake ambao humfwatilia mtandaoni.




Tak. 2: *Novemba 26, 2022. Uk 14*

Tak. 2 inamrejelea mwanamitindo wa nchi ya Wales Alaw Haf akiwa amevalia mavazi meupe huku chini yake kuna maelezo mafupi '*Wales kulishwa asali wakitoboa*'. Picha hii pamoja na maelezo ya kisitiari ni matini za kisemiotiki zinazozua maana zifuatazo:

*Uzalendo kwa nchi yake:* Mwanamitindo huyu alionyesha uzalendo na upendo kwa nchi yake ya Wales kwa kutoa ahadi kwa wachezaji pamoja na mashabiki wa kikosi hicho. Alaw Haf aliahidi kupunguza bei ya picha na video zake za ngono kwa asilimia 50% kwa mashabiki wa nchi ya Wales iwapo wangefaulu kufuzu kwa hatua ya makundi. Hali hii inadhihirisha hisia za mwanamitindo huyu zinazowasilisha ujumbe wa uzalendo. Heather & Noxol (2014) wanaeleza kuwa maana hujitokeza kwa kuzingatia hisia za mtu, imani au mawazo ambayo yameambatanishwa na kiashiria. Hisia hizi zinadhihirika katika matini ya picha ya Tak. 2.

*Kushabiki mchezaji Gareth Bale:* Pia, alitoa ahadi ya kupunguza bei hadi asilimia 75% kwa mashabiki ambao majina yao yalikuwa yanaitwa Gareth ili kuonyesha kuwa yeye ni shabiki sugu wa nahodha wa timu hiyo ya Wales Gareth Bale.

*Kupeana motisha kwa wachezaji wa Wales*: Kando na mashabiki, aliahidi kuonyesha hizo video bure kwa wachezaji wa Wales na pia kuwaahidi kuwapa burudani bure ya kutikisa buyu lake bila malipo yoyote iwapo wangejizatiti ili wafaulu kushinda kombe hilo la dunia 2022. Hii ilikuwa mbinu mojawapo tu ya kuwapa motisha wachezaji hao ili watie bidii katika mashindano hayo na kuleta taji hilo nyumbani.




Tak. 3: *Novemba 26, 2022. Uk 14.*

Kwenye picha ya Tak. 3 tunaona mwanamitindo wa Uhispania Addison Rae akiwa amevalia nguo nyeusi. Kando yake kuna maelezo mafupi '*Addison kuwapa masogora wa Uhispania bonge la burudani wakiiingia fainali*'. Picha hii na maelezo haya ni matini za kisemiotiki kwani ni ishara zinazosetiri jumbe maalum zifuatazo:

*Lugha ya ushawishi kuonyesha uzalendo*: Mwanamitindo alitaka kuwaburudisha mashabiki wa Uhispania kwa kuvua nguo zake na kusalia uchi kama njia mojawapo ya kuonyeha ushabiki wake kwa nchi hio.

*Kupata umaarufu Tik tok*: Pia, mwanamitindo huyu alitumia fursa hii ili kuendelea kujizolea wafuasi wengi katika mtandao wa Tik Tok ili kuendeleza umaarufu wake.




Tak .4: *Desemba 21, 2022. Uk 18*

Tak. 4 ni picha inayotangaza kampuni ya betgr8 ambayo ilitumia mchuano wa finali za kombe la dunia 2022 kati ya Argentina na Ufaransa. Katika picha hii, kuna wachezaji wawili wa timu hizi, Lionel Messi ambaye ni nahodha wa Argentina na Kylian Mbappe ambaye ni nahodha wa Ufaransa. Mbali na kuitangaza kampuni, picha hii ni ishara ya kisemiotiki yenye uzito zaidi:

*Kuongeza uzito na athari ya ujumbe kuhusu kampuni na bidhaa zake*: Messi na Mbappe ni miongoni mwa wachezaji maarufu sana ambao wanajulikana ulimwengu mzima kutokana na vipaji vyao vya kucheza kandanda. Hivyo, kwa kutumia picha za hawa wachezaji inakuwa rahisi kusambaza matangazo kwa watu wengi hasa wacheza kamari pamoja na mashabiki wa kandanda.

*Kutumia lugha shawishi*: Kampuni hii ya betgr8 imetumia lugha shawishi kwa kueka bonasi ili kuwashawishi wawekezaji. Kwa mujibu wa Crystal & Davy (1969), lugha katika matangazo ya bishara ina majukumu mawili ya kufahamisha na kushawishi. Tangazo hili la betgr8 linatumia lugha shawishi kwa kuwa kupeana ofa ya shilingi 100 kwa wale ambao watatumia kanuni ya kuandika neno TAIFA kuna maana kuwa anayejiunga anapata msukumo ili aweze kujiunga kwani jinsi unavyozidi kuongeza pesa ya kuekeza betgr8 ndipo unazidi kuimarisha nafasi ya kushinda hela nyingi. Hivyo, wanatumia lugha ya kupumbaza ili kukosa kuona uwezekano wa kutojishindia katika kiwango mojawapo. Lugha katika tangazo hili imetumiwa kiufundi ili kuashiria ushindi wa moja kwa moja kwa wale wote watakaoshiriki. Goddard (1998) pia alichangia kwa

kueleza jinsi ambavyo matangazo ya biashara huambatanishwa na picha pamoja na lugha inayovutia wasomaji.

*Ishara hii ni onyo kwa waekezaji*: Hata hivyo licha ya kushawishi watu ujisajili, kampuni hii inatoa onyo kwa wale watajiunga kucheza kwa kuwajibika ili wasije wakawa waraibu. Pia, inaonya wale ambao hawajafika miaka 18 kutojiunga kwani watakuwa wanakiuka sheria za mchezo huo. Lugha ya kuonya imetumiwa ili wale watakao shiriki wafahamu kuwa kuna uwezekano wa kupoteza hela iwapo hutazingatia sheria ambazo zimeekwa. Pia, picha ya wachezaji wawili maarufu zimetumiwa ili kuvutia wasomaji kujua kampuni ambayo inafanya haya matangazo. Kuna mchezaji wa Argentina Lionel Messi na mshambuliaji maarufu wa Ufaransa anayeitwa Kylian Mbappe. Hawa ni wachezaji ambao ni tajika sana ulimwenguni na wanatambulika na kila shabiki wa mchezo wa soka.




**Tak .5**: *Novemba 18, 2022. Uk 12.*

Picha ya Tak. 5 inarejelea mshambuliaji wa nchi ya Uswizi Breel Embolo (jezi nyekundu) akikabiliana na kiungo mkabaji wa Cameroon Jean- Charles Castelletto wakati wa michuano ya makundi. Embolo ambaye huchezea klabu ya AS Monaco kule Ufaransa alizaliwa mnamo 14 Februari, 1997 kule Cameroon ila wazazi wake walitengana akiwa na miaka tano na mamake alieza kuhamia kule Ufaransa na kuanza mafunzo ya kucheza kandanda kule Paris. Mamake Embolo alioleka kwa Mswizi na hivyo wakaeza kuhamia kule Basel, Uswizi. Kule Uswizi, Embolo alijiunga na shule ya mafunzo ya wanakandanda chipukizi. Embolo amechezea nchi ya Uswizi tangu akiwa na miaka 16 na amewafungia mabao zaidi ya 30 tangu kuitwa mara ya kwanza. Mnamo mwaka wa 2022, katika mechi yao ya kwanza kwenye kombe la dunia dhidi ya Cameroon, Embolo aliweza kufunga bao la pekee la ushidi dhidi ya nchi zake ambako alizaliwa. Alikuwa mchezaji wa pili kwenye kombe la dunia kufunga dhidi ya nchi yake alikozaliwa ambapo rekodi hii inashikiliwa na Alfred Bickel ambaye pia ni Mswizi baada ya kuifunga nchi yake zaliwa Germany mwaka wa 1938. Kwa ishara ya heshima, Embolo hakusherehekea bao lake na kubeba mikono juu kwa ishara ya kuomba msamaha kwa wananchi wa Cameroon.

Tak. 5 basi ni ishara ya kisemiotiki yenye ujumbe wa usaliti *usaliti kwa nchi zaliwa*: Juu ya picha hii kuna maelezo mafupi 'Cameroon yazimwa na mwana wake' kurejelea huyu mchezaji Embolo ambaye aliigura nchi ya Cameroon kisha akahamia kule Uswizi ambako alianza kucheza kandanda. Wakati wa mchuano huu kati ya Uswizi na Cameroon, Embolo alieza kufunga bao la pekee ambalo liliwapa Uswizi ushindi dhidi ya nchi yake ambako alizaliwa.




**Tak .6**: *Desemba 23, 2022. Uk 20*

Picha ya Tak. 6 inaonyesha wachezaji wa timu ya Argentina wakisherehekea kombe la dunia baada ya kuwapiga Ufaransa kwenye finali. Chini ya hii picha kuna maelezo mafupi '*Ngarambe ya hela nzito*' wakirejelea hela ambazo kila timu ambayo ilishiriki kombe la dunia ilipata baada ya kukamilika kwa mchuano huo. Katika picha hii kuna nahodha wa Argentina akiwa amebeba kombe la dunia huku akiwa na vazi tofauti na wengine. Vazi hili ni spesheli hasa kwa utamaduni wa nchi ya Qatar na Messi alieza kuvalishwa ili kutoa ishara maalum. Vazi hilo linajulikana kama '**Bisht**' na hutengenezwa kwa nyenzo nyepesi, iliyopambwa kwa dhahabu halisi ambayo huvaliwa juu ya kitambaa nyeupe. Kimsingi huvaliwa katika eneo la Ghuba na ni vazi ambalo limevaliwa kwa karne nyingi wakati wa hafla maalum. Kulingana na Pierce (1839-1914) anasema kuwa ishara ni kitu chochote ambacho kinasimama kwa niaba ya kitu kingine. Ishara hubeba maana zaidi ya moja kulingana na Pierce. Kwake, mantiki katika ishara hutegemea tajriba na maarifa ya kijamii ili kufasiri. Ishara hii imo katika kategoria ya tatu kwa mujibu wa Pierce (1996) aliyegawanya ishara katika aina tatu kuu. Kwanza ni alama inayofanana moja kwa moja na kile kinachowasilishwa, pili ni alama yenye uhusiano wa moja kwa moja na sababu na athari ya kile kinachowakilisha na tatu ni ishara ambayo maana yake hujengwa na makubaliano ya kijamii. Picha hii basi ilitumika kama ishara ya kutangaza na kuendeleza utamaduni wa nchi ya Qatar.

Inatazamwa kama ishara ya kuthaminiwa na heshima na kwa kawaida huvaliwa na viongozi wakuu kama vile wanasiasa, masheikh na watu wengine wa hadhi ya juu. Vazi hilo lina maana muhimu sana kwa Waqatari kwani huvaliwa katika hafla rasmi na hutumiwa kwa sherehe. Hassan Al Thawadi, katibu mkuu wa kamati ya maandalizi ya kombe la Dunia Qatar, aliambia BBC Sport 'kumvalisha Messi bisht ni ishara mojawapo ya kuonyesha ulimwengu utamaduni wetu wa Kiarabu na Kiislamu' Hali

hii inashadidiwa na Short (2007) anayeeleza kuwa maana za ishara za kisemiotiki hutokana na mazoea ya jamii pamoja na utamaduni wa jamii husika.

### 4.2. Matini za kitamathali

Mataini za kisemiotiki zilidhihirika kama tamathali za usemi zilizoashiria ujumbe maalum katika magazeti ya Taifa leo kuhusu kombe la dunia 2022. Tamathali zifuatazo zilidhihirika:

#### *4.2.1. Jazanda*

*Asali*: Katika **picha ya Tak .1,** mwandishi ametumia neno '*asali*' akirejelea mwanamitindo Miss BumBum ambaye alitangaza wazi kwamba atampa mchezaji Lionel Messi iwapo watashinda kombe la dunia. Neno hili limetumika kijazanda kwani asali inayorejelewa hapo ni mahaba ambayo mwanamitindo huyu anamwahidi Messi iwapo ataweza kusaidiana timu yake kushinda kombe la dunia 2022. Kisemiotiki, dhana hii hurejelea upendo, furaha ya maisha, bidii kwa kazi na ustahimilivu (Levi-Strauss 1984). Hivyo neno hili limetumika kurejelea mchezaji Lionel Messi ambaye anapewa motisha ya kutia bidii ili nchi yake iweze kunyakua kombe la dunia 2022.

*Wales kulishwa asali:* Katika picha ya **Tak. 2** mwanamitindo Alaw Haf ametumia haya maneno kijazanda kurejelea burudani ya wapenzi wakati ambapo wanafanya mahaba ya chumbani. Mwanamitindo huyo aliyekuwa akionekana amevalia chupi nyeusi na skafu ya Wales alimwahidi nahodha na mshambulizi wa Wales Gareth Bale pamoja na masogora wote wa kikosi hicho 'zawadi spesheli' iwapo watajituma vilivyo na kunyanyua Kombe la Dunia nchini Qatar. Hio zawadi spesheli ilitumiwa kimafumbo kwani aliahidi kupunguza bei ya picha na video zake za ngono mitandaoni kwa asilimia 50% huku akitaka wachezaji wa Wales kujiandaa kuondoa asali ya mzinga wake bila gharama yoyote iwapo wangetwaa ubingwa huo. Pia, aliahidi kumpa Bale asali yake bila kulipia gharama yoyote iwapo wangetinga fainali na kunyakua ushindi. Wanasoka wengine wa Wales waliahidiwa kutikisa buyu hilo la asali bila malipo kila mmoja kwa zamu yake iwapo wangeshinda mchuano huo.


Mastaa wa Denmark watakosa miereka ya chumbani mwezi 1

**Tak .7**: *Novemba 19, 2022. Uk wa 14*

*Uhispania kupewa burudani ya kipekee wakishinda kombe la duni:* Maneno haya yametumiwa kijazanda katika picha **3** kwani kwa mujibu wa gazeti la Taifa Leo, burudani ambayo Addison aliwaahidi wanasoka na mashabiki wa timu ya taifa ya Uhispania ni kuvua nguo na kusalia uchi wa mnyama ili kusherehekea ufanisi huo.

Picha ya **Tak.7** imetumia jazanda kurejelea kanuni ambazo wachezaji wa Denmark walifaa kuzingatia wakati wa kombe la dunia. Wametumia neno '*wachezaji wa Denmark kukosa miereka ya chumbani kwa mwezi mmoja*'. Miereka ya chumbani imetumika kurejelea hisia za wanandoa. Hali ya tamathali za usemi kbainika kama tamathali inashadidiwa na Eco (1976) anayeeleza kuwa ujumbe ambao huwasilishwa kwenye ishara huwa si wa moja kwa moja bali huwa wa kitamathali. Ishara huwa na maana zaidi ambayo hutokana na uhusiano uliopo baina ya ishara na kinachoashiriwa.

### 4.3. Matini za rangi

*Rangi nyeupe*: Katika **picha ya Tak. 1,** maneno *miss Bumbum aahidi Messi asali Argentina ikifana Qatar* yameandikwa kwa rangi nyeupe kwa herufi kubwa ili kuwavutia wasomaji na pia kuweza kuonekana kwa urahisi na wasomaji. Pia, rangi nyeupe huashiria amani ambapo miss BumBum alisema haya maneno kwa kutokuwa na lengo la kuleta vurugu baina ya nahodha wa Argentina Messi na mkewe. Miss BumBum amevalia jezi nambari kumi ya Argentina kuashiria kuwa yeye ni shabiki sugu wa huyu mchezaji na hivyo yuko tayari kumshabikia wakati wa michuano ya Kombe la Dunia.

*Rangi nyekundu*: Picha nzima imekolezwa kwa rangi nyekundu huku chini yake kuna picha ya Messi akiwa anasherehekea. Rangi nyekundu mara kwa mara huonyesha ishara ya mapenzi. Ndio maana siku ya wapenzi husherehekewa kila mwaka mwezi wa Februari tarehe kumi na nne watu wakiwapa wapenzi wao maua mekundu. Hii ni ishara ya mapenzi ambayo huyu mwanamitindo ako nayo kwa mchezaji Messi.

*Rangi ya kijani*: Maandishi katika picha ya **Tak. 2** '*Wales kulishwa asali wakitoboa*' yameandikwa kwa rangi ya kijani ili kuonekana vizuri na kuwavutia wasomaji. Rangi ya kijani zaidi hurejelea mazingira na huwa kivutio sana na kufanya manthari ya mahali yawe shwari. Hii inarejelea nyuki ambao hutegemea maua ili kuweza kuunda asali ambayo huwa tamu sana baada ya kuundwa. Asali hii inarejelea buyu la Alaw Haf kuwa tamu na ni ndoto ya kila mwanaume kuonja.

*Rangi nyeusi*: Juu ya picha ya Tak. **2** kuna maandishi ya rangi nyeusi ikieleza kazi ya huyu mwanamitindo kuwa *yeye ni kahaba muuza picha na video za uchi mitandaoni*. Rangi nyeusi mara nyingi hurejelea matendo maovu ambayo hayakubaliwi katika jamii. Alaw Haf ni kahaba wa kuuza picha zake akiwa uchi ambayo ni tabia hasi isiyokubalika katika jamii nyingi ulimwenguni kote. Mwanamke hafai kutumia mwili wake ili kupata pesa bali anahimizwa kutia bidii ili kupata hela ambazo ni halali na kwa njia inayofaa. Mutiso (1996) anasema kuwa rangi nyeusi inahusishwa na giza ambalo linahusishwa na mambo kama vile uchawi, uoga, kushindwa, upweke,

msiba, mashetani, mizuka, ujinga miongoni mwa mambo mengine. Madai haya ni ya kweli kwa kuwa rangi nyeusi inahusishwa na maovu. Kwa u pande mwingine, amevalia nguo nyeupe kuonyesha amani wala hana nia yoyote mbaya ya kuvunja uhusiano wa wachezaji wa Wales na wachumba wao. Pia, amevalia vazi la rangi nyeupe ili aweze kuonekana vizuri na kuonyesha maumbile yake yanayovutia.

*Rangi nyinginezo*: Picha ya Tak. 4 imetumia rangi mbalimbali wakati wa matangazo ya kampuni ya kamari ili maandishi haya yaweze kuonekana vizuri na pia kuwavutia wasomaji. Kwa mfano, kuna nyeupe pamoja na nyekundu kwa maneno 'bet' na 'gr8' mtawalia ili kufahamisha waekezaji kujua ni kampuni ipi inarejelewa kwa urahisi. Rangi nyekundu huwa rahisi kuonekana na hivyo ilitumiwa kimakusudi ndipo wacheza kamari waweze kuona kwa urahisi. Pia, njisi ya kujisajili pamoja na bonasi ambazo wanapeana zimeandikwa kwa *rangi tofauti tofauti* kwa lengo la kuonekana na kuwavutia wasomaji wa gazeti la Taifa leo. Rangi mbalimbali hutekelezi wajibu mkubwa katika kazi za fasihi ili kuashiria mambo ambayo uhalisia wake hujitokeza katika maisha ya binadamu. Heather na Noxol (2014) wanaeleza kuwa maana hujitokeza kwa kuzingatia hisia za mtu, imani au mawazo ambayo yameambatanishwa na kiashiria. Vitu kama rangi, nguo, maneno au ishara za kimwili huchangia pakubwa hadhira inapofasiri maana katika ishara. Matumizi ya rangi kama vile nyekundu katika kusimba maana kunaleta uhalisia wa hatari, huzuni, uhai au kifo. Rangi nyekundu ni ishara ya uhai na vile vile ya tahadhari, hatari ya kifo, kwa kuwa bila damu mwili huna uhai. Vile vile rangi nyekundu huonewa huashiria matajiri wanavyoionea fahari hali yao ya utajiri kulingana ya madai ya Mberia (1997). Rangi ni mojawapo ya ishara ambazo kwa mujibu wa Pierce (1996) huwa na uhusiano wa moja kwa moja na kile kinachowakilishwa. Hivyo, kila rangi ina jambo inayowakilisha.

Hizi ndizo alama ambazo msomaji hutumia kutambua dhana au maana inayowasilisha kwa kuzichambua vikamilifu. Pia, ishara huchanganuliwa kwa kiwango cha maelezo bila kuchunguza kwa kina maana inayokusudiwa. Picha huweza kuelezwa bila kuitathmini au kutoa maelezo ya ndani. Hivyo, tunaweza kupata maana kwa kurejelea matini. Semiotiki hutazama ishara kama fumo mpana, na maana haipo ndani pekee bali hupatikana kutokana na uhusiano wake na alama nyingine katika mfumo huo.

Jinshun (2019), anasema kuwa tafiti za semiotiki huzingatia mfumo wa kanuni zinazotawala matini, zikisisitiza dhima ya muktadha wa semi katika kuunda maana. Muktadha huangazia mazingira ya kijamii, kiutamaduni, kihistoria au kijamii. Hii ina maana kuwa ishara moja inaweza kuwa na maana nyingi au tofauti kulingana na mazingira ambamo imetumiwa. Semiotiki huzingatia muundo wa matukio ya kuleta maana, kwa ishara (ya maneno au isiyo ya maneno) kitengo cha msingi. Ishara (k.m. maneno, mavazi) huchanganyika na kuunda ujumbe kwenye matini.

Hivyo, tunatambua kuwa ishara za Kisemiotiki hupata maana kwa misingi tofauti. Muhimu ni kuzingatia muktadha ambamo ishara imetumika ili kufasiri ujumbe unaowasilishwa kwa njia mwafaka.

## 5. Hitimisho na mapendekezo

Matini za kombe la dunia 2022 katika Magazeti ya Taifa Leo zilitumia ishara nyingi za kisemiotiki ambazo zilikuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha ujumbe uliopitishwa kwa wasomi na mashabiki wa soka. Ishara zilizotumika ni picha, rangi, maandishi yaliyo kwenye mavazi na maelezo yaliyoambatanishwa na picha. Ishara hizi zilisetiri maana ambazo hueleweka kulingana na muktadha ambamo zimetumika. Aidha zilisaidia hadhira kuelewa ujumbe vizuri kwa kueleza ujumbe kwa ufupi. Ina maana basi kuwa ishara kwenye vyombo vya habari kama vile gazeti huwa na maana na huchangia kufaulisha ujumbe unaopitishwa. Utafiti unapendekeza kuwa waandishi waweze kuimarisha sanaa katika uandishi kwa kutumia mitindo anuai ya kisemiotiki kuwasilisha jumbe mbalimbali. Vilevile, wasomaji wawe makini zaidi kwa kutumia vigezo vingine vya kufasiri jumbe katika magazeti kama vile kigezo cha pragmatiki na semantiki. Semiotiki ni moja wapo tu wa mikabala ya uchanganuzi wa matini (Jinshun, 2019). Ili kuhakikisha uwasilishaji wa ujumbe kamili kwa hadhira, utafiti unapendekeza kuwa ufasiri wa kitaaluma na wa kina ufanyiwe makala maalum katika magazeti na vyombo vingine vya habari.

## Marejeleo


Alvarez,M.E(2013). Semiology: Pathophysiology,Semiotics and Editorial Media Pa Americana

Arackal, F. (2015). Semiotic and media content. Manuscsript. [Uploaded 2016 on Researchgate]

Barthes, R (1957). Mythologies. New York. Hill & Wang

Barthes, R (1967). Elements of Semiotics (Trabs. Annette lavers and Colins Smith). London: Jonathan Cape.

Barthes, R (1980). Camera Luida: Reflections on photography. (Trans. Richard Howard). New York. Hill and Wang.

Crystal, D. Na Davy, D. (1969). Investigating English style. London, Longman Publisher

Derrida, J (11997). Semiotiki ya alama, logocentrism,differance.

Eco, U. (1976). A theory of Semiotics. London. Macmillan publishers

Eco, U. (1979). A theory of semiotics. Bloomington, IN: Indiana University Press

Eco, U (1996). A Theory of Semiotics. Bloomington. Indiana University Press

Ennon (1998). Qualitative Research and Evaluation methods (3rd ed.). thousand Oaks, CA: Sage

Goddard,C. (1998). An Introduction to the study of semiotics. London: Routledge

Gazeti La Taifa Leo (2022). 18/11/2022. Nation Media Publishers. Nairobi.

Gazeti La Taifa Leo (2022). 19/11/2022. Nation Media Publishers. Nairobi

Gazeti La Taifa Leo (2022). 20/11/2022. Nation Media Publishers. Nairobi

Gazeti La Taifa Leo (2022). 25/11/2022. Nation Media Publishers. Nairobi

Gazeti La Taifa Leo (2022). 26/11/2022. Nation Media Publishers. Nairobi

Heather &Noxol (2014). A Semiotic Phenomenology of Homelessness and the Precarious Community. A Matter of Boundary. PhD dissertation, University of South Florida.

Jinshun L. (2019). Semiotic study of English Texts. Advanced in Social Science Education and humanities Research. V ol.342:312-377.

Kress, G. (2010). Multimodality: A social semiotic approach to contemporary

communication. London: Routledge.

Kress,G & Leeuwen,T (1996). Reading images: The grammar of visual design. London: Routledge

Kress,G & Leeuwen,T (2010). Muitimodal discourse: The modes and media of contemporary communication.

Levi- Strauss,C (1984). Myth and meaning: Cracking the mode of culture. New York: Schocken Books.

Manovich,L (2001). The language of new media. MIT Press.

Wa Mberia, K (1997). Mchezo wa Karata. Nairobi :Marimba Publications Limited.

Wa Mutiso, K (1996). Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry. Kasida ya Burudai (Tasnifu ya PhD ambayo haijachapishwa) Chuo kikuu cha Nairobi.

Noxol(2014). A Semiotic Phenomenology of Homelessness and the Precarious Community. A Matter of Boundary. PhD dissertation, University of South Florida.

Palinkans,L.A (2015). Purposiful sampling for Qualitative Data Collection and Analysis in Mixed Method Implementation Research. Administrative and policy in Mental Health and Mental Health Services Research,42(5) 533-544

Pierce, C.(2002). Elements of Logic. Grammatica Speculativa // Semiotics: Anthology. M. Academichesky Project; Ekaterinburg.

Pierce, C.S. (1996). The essential Pierce: Selected philosophical Writings,volume 2 (1893-1913). Edited by Nathan Houser, Christian Kloese and Jame Edward Cook

Robert, S (2007). Structuralism and Literature London: May Field Publishing company

Sanja, L & Mbuthia,E.(2025). Uchunguzi Kisemiotiki wa Athari za Kihistoria na Kimazingira kwa Uchumi wa Maisha ya Kijamii katika Pwani ya Kenya. Jarida la Kiswahili sainfu, Vol.2 No.1 https://doi.org/10.61889/jakisa.V2i188

Saussure,F.de. (1946). Course in General Linguistics. (Trans. Roy Harris) London. Duckworth

Saussure,F.de. ( 1986). Course in General Linguistics. (Trans. Roy Harris) London: Duckworth

Short,T.L. (2007). Semiotics . The Basis. Routledge

Sign, R & Nity, L (2017). Language contact and borrowing. Sign language: An International handbook (pp. 841-861). Berlin,Germany.